# RIPOTI YA UTAFITI WA WATALII WA KIMATAIFA WANAOONDOKA NCHINI, 2023
# MUHTASARI









## Utangulizi

Sekta ya utalii ya Tanzania inaendelea kuwavutia watalii kutoka kote duniani kutokana na uzuri wake wa asili usio na kifani, urithi wa kitamaduni na uzoefu mbalimbali. Pamoja na mipango inayoendelea ya uhifadhi, na uboreshaji wa miundombinu, Tanzania itabaki kuwa ni nchi inayovutia watalii wanaopenda adventure, wanyamapori, na shughuli za kiutamaduni kwa miaka mingi ijayo.

Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii, Wizara ya maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalli ya Zanzibar, wamekuwa wakifanya tafiti za watalii wa kimataifa wanaoondoka nchini na kutoa ripoti za tafiti hizo kila mwaka.

### Madhumuni

Lengo kuu la tafiti hizi ni kukusanya taarifa sahihi za mapato yanayotokana na utalii kwa ajili ya takwimu za pato la taifa na urari wa malipo, kutangaza utalii, utungaji wa sera na kupata taarifa za msingi za uanzishwaji wa mfumo wa takwimu za utalii utakaowezesha kukadiria mchango wa sekta ya utalii kwenye pato la taifa.

### Eneo la Utafiti

Hii ni ripoti ya 23 tangu kuanzishwa kwa tafiti hizi ambazo hufanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana na watalii. Mahojiano yalifanyikia katika viwanja vikubwa vitatu vya ndege vya kimataifa, ambavyo ni Julius Nyerere International Airport, Abeid Amani Karume International Airport, Kilimanjaro International Airport, na vituo vitano vya mipakani vya Horohoro, Namanga, Tunduma, Mutukula na Manyovu.

Utafiti huu ulifanya kwa kipindi cha wiki mbili kuanzia tarehe 27 Agosti hadi tarehe 11 Septemba 2023 na kukusanya maoni kutoka wa watalii 12,372 waliowakilisha mataifa 123. Utafiti ulifanyika katika kipindi hichi kwa sababu ni msimu mkuu wa watalii.


## Matokeo Muhimu ya Utafiti

### Utalii wa Kimataifa Kunaendelea Kuimarika

Mwaka 2023, utalii wa kimataifa ulifikia asilimia 88 ya viwango vya kabla ya janga la UVIKO-19, sawasawa na wageni bilioni 1.3, kama ilivyoripotiwa na shirika la UNWTO World Tourism Barometer ya Januari 2024 (**Kielelezo Na. 1**). Kuimarika kwa sekta kulitokana na kuendelea kupungua kwa janga la UVIKO-19, kuendelea kupanuka kwa teknolojia, pamoja na juhudi za kuleta maeneo anuwai.

**Kielelezo Na. 1: Kuwasili kwa watalii wa kimataifa, 2012-2023**

Milioni





Chanzo: UNWTO Barometer 2024 (Januari)

### Mapato ya Utalii yaliongezeka

Kwa upande wa Tanzania, sekta ya utalii imeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa, kutokana na ongezeko la idadi ya watalii pamoja na matumizi yao hapa nchini. Mapato yatokanayo na utalii kwa mwaka 2023 yaliongezeka kwa asilimia 33.5 hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,373.8 kutoka dola milioni 2,527.8 mwaka 2022. Sambamba na hilo, idadi ya wageni wa kimataifa iliongezeka kwa asilimia 24.3 hadi kufikia 1,808,205 - rekodi ya juu zaidi kuwahi kufikiwa—mwaka 2023, ikilinganishwa na watalii 1,454,920 kwa mwaka 2022 (**Kielelezo Na. 2**).

**Kielelezo Na. 2: Mapato ya Utalii na Idadi ya Watalii walioingia Nchini**





***Matumizi ya Mtalii kwa siku yaliongezeka***

Wastani wa matumizi ya mtalii kwa siku ulikuwa dola za Marekani 250 kwa mwaka 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani 214 mwaka 2022, hivyo, kuendelea kuakisi kuimarika kwa sekta ya utalii. Kwa Zanzibar, wastani wa matumizi ya mtalii ulikuwa dola za Marekani 257 kwa mtalii kwa siku, ikilinganishwa na dola za Marekani 218 zilizorekodiwa mwaka 2022 (**Kielelezo Na.3**)

**Kielelezo Na.3: Wastani wa Matumizi ya Fedha kwa Mtalii kwa siku**

Dola ya Marekani




**Matumizi ya mtalii kwa kulipia kwa vifurushi kabla ya kuingia nchini yaongezeka**

Mwenendo wa wastani wa matumizi ya watalii waliokuja kwa kulipia kwa vifurushi kabla ya kuingia nchini umekuwa ukiongezeka zaidi ukilinganisha na wastani wa matumizi ya watalii waliofanya malipo wakiwa wamefika nchini Tanzania (**Kielelezo Na. 4**).

**Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Mtalii, 2018 – 2023**

Dola ya Marekani





*Marekani imekuwa chanzo kikuu cha watalii nchini Tanzania*

Nchi zilizoongoza kuleta watalii wengi Tanzania ni Marekani, ikifuatiwa na Italia na Ujerumani. Sawia na mwaka 2022, nchi hizi zimeendelea kuwa chanzo kikuu cha watalii hapa Tanzania. (**Kielelezo Na. 5**).

**Kielelezo Na. 5: Nchi 15 Zilizoongoza Kuleta Watalii Tanzania**

Asilimia





Kongo* – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
UFK* – Umoja wa Falme za Kiarabu

Kwa upande wa Zanzibar, Italia ilirudi kwenye nafasi yake ya kwanza ya kuongoza kuleta watalii wengi baada ya kushuka katika nafasi hiyo tangu mwaka 2016. Masoko mengine muhimu ni pamoja na Ujerumani, Ufaransa na Uingereza. Masoko 15 muhimu yalichangia wastani wa asilimia 78 ya wageni wote waliotembelea Zanzibar kwa Mwaka 2023 (Kielelezo Na. 6).

**Kielelezo Na.6: Nchi 15 Zilizoongoza Kuleta Watalii Zanzibar**

Asilimia





## *Masoko ya Zambia, Kenya na Ethiopia yaliongoza katika bara la Afrika*

Katika bara la Afrika, watalii wengi waliotembelea Tanzania walitoka Zambia, Ethiopia na Kenya. Hii imechangiwa na ushirikiano wa kikanda na mahusiano mazuri ya kibiashara (**Kielelezo Na. 7**).

**Kielelezo Na.7: Watalii waliotembelea Tanzania kutoka bara la Afrika**

Asilimia




**Wageni wengi walikuja Tanzania kwa ajili ya burudani na mapumziko**

Watalii wengi waliotembelea Tanzania walikuja kwa ajili ya burudani na mapumziko, wakifuatiwa na waliokuja kwa ajili ya kutembelea ndugu, jamaa na marafiki pamoja na kufanya biashara (**Kielelezo Na. 8**). Wageni wengi kuja kwa ajili ya mapumziko na kufanya biashara kwa kiasi kikubwa, kunaonyesha jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali katika kutangaza utalii pamoja na kuongeza fursa za biashara na uwekezaji nchini.

**Kielelezo Na. 8: Mchanganuo wa Watalii kwa Madhumuni ya Safari**

Asilimia




***Wanyamapori waendelea kuwa kivutio kikubwa kwa watalii***

Wanyamapori, fukwe, kutembelea ndugu, jamaa na marafiki na kufanya biashara ndio shughuli zilizowavutia watalii wengi hapa nchini. Shughuli hizi zimekuwa zikivutia wageni zaidi kwa miaka mitatu mfululizo, wanyamapori wakichukua nafasi kubwa zaidi ya asilimia 41.5 mwaka 2023.





Kwa upande wa Zanzibar, utalii wa fukwe na utamaduni uliendelea kutawala.




***Ngorongoro, Serengeti, Pwani, Mji Mkongwe na Tarangire ndio vivutio vilivyotembelewa zaidi***

- Vivutio vilivyotembelewa zaidi ni Ngorongoro, Serengeti, Pwani, Mji Mkongwe na Tarangire, vikiwa na takriban asilimia 56 ya maeneo yote yaliyotembelewa.
- Maeneo haya yalitembelewa zaidi na watalii kutoka masoko ya Marekani, Ujerumani, Italia, Ufaransa na Uingereza.
- Umaarufu wa Ngorongoro, Serengeti na Tarangire unatokana na sura za kipekee ya maeneo haya ambayo ni pamoja na Bonde la Ngorongoro lenye kuvutia - eneo kubwa zaidi duniani, uwepo wa wanyamapori wengi wanaotembea kwa uhuru na uhamiaji maarufu wa kila mwaka wa nyumbu, pundamilia na swala.
- Zaidi ya hayo, umaarufu wa fukwe za mchanga mweupe na Mji Mkongwe unachangiwa na historia nzuri ya Zanzibar.










***Wageni wenye umri wa miaka "25 – 44" waliendelea kutawala***

Asilimia kubwa ya wageni waliokuja nchini mwaka 2023 walikuwa katika kundi la umri wa miaka 25 – 44. Watalii wenye umri wa chini ya miaka 18 na wenye umri wa miaka 65 na zaidi waliendelea kuwa wachache. (**Kielelezo Na. 10**).

**Kielelezo Na. 10: Wageni kwa Kundi la Umri**

Asilimia



## Ukarimu wa watanzania na mapokezi mazuri yanawafanya watalii wengi waipende Tanzania

Watanzania kwa asili ni watu wema na wakarimu, jambo ambalo kwa miaka mingi limekuwa likiwavutia watalii wengi wanaotembelea nchini. Urithi wa nchi katika wanyamapori na mandhari nzuri pia ni pamoja ya sifa za kushangaza na za kuvutia kwa watalii, ikiwa ni pamoja na chakula kitamu na cha asili (**Kielelezo Na. 11**).

**Kielelezo Na.11: Mtazamo wa Wageni Kuhusu Soko la Utalii la Tanzania**

Asilimia

